# Hali ya Lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu nchini Tanzania: Mifano kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

**Sauda Uba Juma & Editha Adolph**
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2023-09-12*
*Rekebishwa: 2023-11-23*
*Kubalika: 2023-12-30*
*Chapishwa: 2023-12-31*

***Maneno Muhimu***
Lugha
Kiswahili
Kongamano
Vyama

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Adolph, E., & Juma, S. U. (2023). Hali ya Lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu nchini Tanzania: Mifano kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 1(2), 43-53.

*Copyright © 2023*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Watafiti wa makaka hii wanaangazia hali ya lugha ya Kiswahili katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA[1] kuanzia sasa). Azma ya uchunguzi huo ni kutaka kubaini endapo lugha ya Kiswahili inapewa nafasi stahiki katika Chuo hicho au la. Hii inatokana na ukweli kwamba kuna baadhi ya taasisi ambazo zinaithamini sana lugha ya Kiswahili na kuipa nafasi sawa na lugha nyingine za kigeni. Hata hivyo, zipo baadhi ya taasisi ambazo zinaibeza lugha hii na kuiona kama kwamba haina nafasi yoyote kitaaluma na kimawasiliano. Data ya makala hii imekusanywa kupitia njia tatu: upitiaji wa nyaraka mbalimbali kutoka maktabani, usaili na ushuhudiaji. Hivyo, njia zote hizo kwa pamoja zimetusaidia kupata data faafu na ya kutosha kulingana na malengo ya makala hii. Vilevile, uchambuzi wa data katika utafiti huu, umetumia mkabala wa kitaamuli ambapo mbinu za kimaelezo na kiufafanuzi zimetumika katika kudadavua vipengele mbalimbali ambavyo vimebainishwa. Sanjari na mkabala huo, tumetumia pia mkabala wa kitakwimu ambao kimsingi umejikita katika uchambuzi wa data kwa kutumia namba. Mkabala huu ulitumika pale tu ilipobidi kufanya hivyo ili kuonesha idadi ya baadhi ya vipengele vilivyokuwa na uhitaji huo. Aidha, matokeo yameonesha kwamba, kuna mabadiliko na mafanikio makubwa MNMA katika kuikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili, tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Tunadiriki kusema hivyo kwa kuwa tumebaini juhudi lukuki za makusudi zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa kwa minajili ya kuikuza na kuiendeleza lugha hii ya Kiswahili.

## Utangulizi

Kiswahili kinaaminika kuwa chanzo chake ni Uswahilini yaani pwani ya kaskazini mwa Kenya kati ya Lamu na mahala ambapo mto Tana huingia baharini. Kilienea kusini mwa Mombasa, Unguja, Kilwa na kaskazini kuelekea upande wa Mogadishu katika nchi ya Somalia. Athari za Waarabu kwa Waswahili zilianza katika karne ya 9 na 10 (Mbaabu, 2007). Inakisiwa kuwa lugha hii ina takribani wazungumzaji zaidi ya milioni 60 kote ulimwenguni (Massamba, 1995). Lugha hii pia imepiga hatua katika elimu kwa kuwa hufundishwa katika vyuo vikuu zaidi ya 100 nje ya Afrika (Kamwendo, 2000).

[1] The Mwalimu Nyerere Memorial Academy.

Aidha, Kiswahili ni lugha rasmi na ya taifa nchini Tanzania na Kenya (Mazrui, 1995). Kutokana na hali hiyo, Kiswahili kinatumika katika nyanja mbalimbali za maisha kama vile siasa, elimu, biashara, dini, vyombo vya habari, bungeni na kadhalika.

Hivyo, lugha ya Kiswahili imebeba majukumu muhimu katika jamii. Kutokana na majukumu hayo, wanazuoni na watafiti mbalimbali wamejikita katika kuichunguza lugha hii kwa undani zaidi. Miongoni mwa wanazuoni waliofanya utafiti kuhusiana na lugha ya Kiswahili ni: Morani (2007) alifanya utafiti kuhusu hali ya Kiswahili nchini Kenya. Katika utafiti wake anadai kwamba ni jambo la kusikitisha kuona lugha ya Kiswahili haijapewa hadhi ya kutosha nchini Kenya kama ilivyo Tanzania. Tanzania hutumiwa kufundishia masomo yote katika shule za msingi. Vilevile, Marshad (1993) na Chimera (1998) wanadai kwamba Kiswahili hakijafikia kiwango kinachostahiki kinapolinganishwa na Kiingereza katika nyanja tofauti za maisha. Kwa maoni yao hali hii imetokana na sera inayoyumbayumba ya lugha na kasumba ya ukoloni.

Naye Mjawiri (2016) alifanya utafiti kuhusu hali ya Kiswahili Zanzibar na mustakabali wake. Lengo la makala yake ni kutathmini hali halisi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili Zanzibar kwa kuangalia sera zinazohusiana na lugha. Aidha, utafiti wake umejikita katika kuchunguza hali ya utendaji wa taasisi hizo na matumizi ya Kiswahili katika ofisi za umma. Ofisi zilizobainishwa ni: Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (SKILUKI), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo (WHUUM). Taasisi hizo ndizo zinazohusiana na kukuza na kusimamia lugha ya Kiswahili Zanzibar. Utafiti wake umebaini kwamba kuna juhudi mbalimbali zinazofanywa na taasisi hizo katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili. Pamoja na juhudi hizo utafiti wa Mjawiri ulibaini kwamba bado Kiswahili hakijapewa hadhi yake stahiki dhidi ya Kiingereza. Hivyo, alipendekeza kwamba lugha ya Kiswahili itumike katika kufundishia shule za upili kama asemavyo:

> Kila mtu anafahamu kuwa ukimsomesha mtu kwa lugha yake anafahamu na kutafakari zaidi katika mbea zote za makuzi na mawasiliano (Mjawiri, 2016, p. 25).

Wataalamu wengine ambao wamefanya tafiti kadhaa juu ya ukuaji, ueneaji na fursa mbalimbali zitokanazo na lugha hii adhimu ya Kiswahili ni pamoja na: Gibbe (1983), Mazrui na Shariff (1994), Mazrui na Alamin (1998), Massamba (2007), Maganga (2008), Matei (2008), Mutembei (2011), Odeo na Wamalwa (2017) na Adolph (2023). Kwa ujumla wataalamu hawa wanasema kuwa lugha ya Kiswahili imekua na kuenea ulimwenguni kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wake, kukua kwa msamiati wake, kupewa kipaumbele katika nchi mbalimbali na kadhalika. Aidha, Kiswahili kinatoa fursa mbalimbali kwa watumiaji wake na watumiaji wa lugha nyingine kama vile: tafsiri, ukalimani, uchapaji na uchapishaji, uandishi wa vitabu na uuzwaji wake, ufundishaji na kadhalika.

Nao Mark na Jacktone (2014) walichunguza namna Kiswahili kinavyotumika kama chombo cha kutangaza na kuuza vyombo vya habari nchini Kenya. Kwa ujumla wanasema kuwa kufikia mwaka 1999, vituo vya redio nchini Kenya vilikuwa 10 pekee. Mwaka 2004 idadi hiyo iliongezeka na kufikia 118. Idadi kubwa ya vituo hivi imeongezeka kuanzia mwaka 2000 wakati sekta ya habari na utangazaji ilipowekwa huru kutokana na masharti ya utoaji wa masafa ya kutangazia kulegezwa na hivyo kuwaruhusu wamiliki binafsi kuanzisha vituo vya redio. Aidha, wanaeleza kuwa vituo mbalimbali hutoa matangazo yake kwa kutumia Kiswahili. Hii inatuthibitishia wazi kuwa Kiswahili kinatoa fursa ya ajira kupitia vyombo vya habari.

Adolph (2023) ametafiti juu ya fursa mbalimbali zitokanazo na Kiswahili. Mtafiti huyu ameangazia fursa zitokanazo na Kiswahili nchini Tanzania zilizooneshwa na viongozi mbalimbali katika maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani (MASIKIDU) iliyofanyika 7/7/2022. Miongoni mwa viongozi aliowarejelea ni pamoja na Mh. Philip Mpango Makamu wa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia kiongozi huyu, Adolph (keshatajwa) anaonesha fursa nyingi mathalani, shughuli za tafsiri, uigizaji, uhariri, ukalimani, uchapishaji, ufundishaji pamoja na uandishi wa vitabu. Zaidi ya hayo, kiongozi huyu anasisitiza kuwa Kiswahili ni nyenzo muhimu kwa mawasiliano, kufanya biashara, kujenga umoja na maelewano, pamoja na utalii.

**Mbinu za Utafiti**

Data ya makala hii ilikusanywa katika vyanzo mbalimbali kuhusu hali ya lugha ya Kiswahili MNMA. Kwa ujumla njia tatu zilitumika katika kukusanya data. Mosi, udurusu wa nyaraka mbalimbali maktabani, makavazini na kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii ili kupata zinazohusu mafanikio pamoja na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili MNMA. Nyaraka hizo zimejumuisha machapisho mbalimbali kama vile vitabu, kamusi pamoja na tafiti mbalimbali ambazo zimehusiana na suala hilo. Vilevile, mbinu hii ya upitiaji wa nyaraka, imetumika ili kuhakiki data iliyopatikana kupitia njia ya usaili.

Mbinu ya pili iliyotumika ni usaili ambapo watafiti walionana ana kwa ana na baadhi ya wafanyakazi, wahadhiri/wahadhiri wasaidizi pamoja na wanafuzi kwa ujumla. Watafitiwa walisampulishwa maksudi ili kupata watu wa kutoa data ya kutegemewa.

Mbinu ya tatu ilijumuisha ushuhudiaji wa matukio mbalimbali yanayofanyika MNMA kila uchao. Ushuhudiaji ni mchakato wa kukusanya data ambapo mtafiti hushuhudia jambo analolitafiti kwa kuangalia na kusikiliza ili kupata taarifa. Walliman (2011) anaeleza kwamba ushuhudiaji ni mbinu ya kurekodi hali, matukio na shughuli kwa njia ya kutazama kwa kutumia milango ya fahamu au vifaa maalumu kama vile kamera, tepurekoda, na darubini. Kupitia njia hii ya ushuhudiaji, watafiti walikusanya data kwa kutumia kamera, kinasa sauti na pia kunakili katika daftari waliyoyashudia. Hii ndiyo data iliyochanganuliwa na ambayo kwayo matokeo ya utafiti yaliegemezwa.

**Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa msingi wa lengo la makala hii ambayo ni kuangalia hali ya lugha ya Kiswahili katika MNMA kama ifuatavyo:

**Mafanikio**

MNMA kimeweza kuimarisha Kiswahili na kukipa nafasi ya juu kutokana na mambo mbalimbali yanayotekelezwa. Miongoni mwa mambo hayo ni matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano, upanuzi wa kozi, ongezeko la wahadhiri, kuanzishwa kwa Idara ya Lugha na Fasihi, kufanyika kwa tafiti mbalimbali za kitaaluma, udhamini wa masomo, ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa kila mwaka pamoja na mchango wa wahadhiri katika makongamano na vyombo vya habari. Mafanikio yote hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo.

**Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano**

Mojawapo ya mafanikio yaliyopatikana MNMA, ni kuwepo kwa uhuru wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mawasiliano ya kila siku. Hii inatokana na ukweli kwamba, hapo awali Chuo hicho hakikutilia sana maanani suala la matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano rasmi na wakati mwingine hata yasiyo rasmi. Hapo awali Kiingereza kilipewa nafasi kubwa ambapo kilionekana kuwa na hadhi zaidi kikilinganishwa na Kiswahili. Hivyo, baadhi ya wafanyakazi pamoja na wanafunzi walipenda kukitumia zaidi hasa katika mawasiliano rasmi. Hivi sasa ni jambo la kujivunia

kuona kwamba, Kiswahili kinatumika katika miktadha mbalimbali. Mathalani, kwenye vikao mbalimbali vinavyojadili mambo yanayohusu mustakbali wa Chuo, barua zinazoandikwa na watumishi kwa ajili ya maombi ya stahiki zao kadha wa kadha.

Aidha, Kiswahili kinaruhusiwa kutumika kwenye kongamano ambalo linafanywa chuoni hapo kila mwaka ifikapo mwezi wa Oktoba. Kongamano hilo hufanywa kwa minajili ya kumbukizi ya Baba wa Taifa Marehemu Raisi Julius Kambarage Nyerere ambaye ndiye aliyekuwa Raisi wa kwanza wa Tanzania. Hivyo, kwa kuwa Raisi Nyerere ndiye mwanzilishi wa MNMA kwa mnasaba huo, Chuo huandaa kongamano na kuwaalika watu maarufu, wanasiasa na jamii kwa ujumla ili kuhudhuria kongamano hilo. Kwa kawaida mada mbalimbali zinazomhusu Raisi Nyerere zinawasilishwa. Mada hizo zinaruhusiwa kuandikwa kwa Kiswahili au Kiingereza. Bila shaka kuwepo kwa uhuru wa matumizi ya Kiswahili, kumewakomboa sana Watanzania walio wengi. Hii inatokana na ukweli kwamba, kunawapa uhuru wa kuitumia lugha yao ya Kiswahili kwa kujiamini zaidi. Tunaelewa fika kwamba, kuna Watanzania ambao Kiswahili ni lugha yao ya kwanza na wengine ni lugha yao ya pili. Hivyo, ni ukweli usio shaka kwamba Kiingereza ni lugha ngeni kwa Watanzania kwa kuwa ni lugha yao ya pili au ya tatu. Bila shaka kutoa uhuru wa kukitumia Kiswahili kunawapa faraja zaidi kwani baaadhi yao, hawana umilisi wa kutosha wa kukitumia Kiingereza kwa uhuru na kujiamini mbele ya umati wa watu.

**Upanuzi wa Kozi**

Hivi sasa kozi za Kiswahili zimepanuliwa MNMA tofauti na ilivyokuwa awali. Hapo awali Kiingereza kilipewa kozi nyingi chuoni kuliko Kiswahili. Kozi zimepanuliwa katika pande zote za isimu na fasihi ili kutoa fursa kwa wanafunzi kuchagua kozi wanazozipenda hasa zile za ihari. Vilevile, upanuzi huo wa kozi umewawezesha wanafunzi wa Kiswahili kumudu na kufurahia masomo yao sambamba na wenzao wanaochukua kozi za Kiingereza. Jambo hili limewapa faraja sana wanafunzi kwa kujiona wako sawa na wenzao kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Baadhi ya wasailiwa walitueleza kwamba, Kiswahili kilitwezwa sana kiasi ambacho kozi zake zilikuwa chache mno zikilinganishwa na zile za Kiingereza. Kutokana na hali ilivyokuwa huko nyuma, wanafunzi waliochagua kusoma kozi za Kiswahili walidharauliwa mno.

Zaidi ya hayo, upanuzi wa kozi MNMA umetoa mshawasha mkubwa kwa wanafunzi kuongezeka kwa wingi kwani huchagua kusoma kozi mbalimbali za Kiswahili kwa uhuru na uwazi bila kuona aibu kama ilivyokuwa hapo kabla. Vilevile wahadhiri wa Kiswahili kwa sasa wanathaminiwa kutokana na utaalamu wao.

Wahadhiri hao, pamoja na kwamba walisomea kozi za Kiswahili, walilazimishwa kufundisha kozi zingine za Kiingereza. Hii ilisababishwa na ufinyu wa kozi za Kiswahili zilizokuwepo MNMA kwa wakati huo. Hali hii iliwavunja moyo sana wahadhiri/wahadhiri wasaidizi na waandamizi ambapo walijiona duni na kwamba walipoteza muda wao bure kusoma kozi za Kiswahili ambazo hawakupata fursa ya kuzifundisha. Hivi sasa walimu wanafundisha kulingana na ubobezi wao katika kozi za isimu na fasihi ya Kiswahili. Hili lilifanikiwa baada ya MNMA kupendekeza mtaala mpya ambao uliidhinishwa na kupitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. (The National Council for Technical and Vocational Education and Training ambapo kwa Kiswahili linajulikana kama Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi Stadi-NACTVE).

**Ongezeko la Wahadhiri**

MNMA kimefanikiwa kuwa na ongezeko kubwa la wahadhiri, wahadhiri wasaidizi na wahadhiri waandamizi ambao wamebobea katika kozi mbalimbali za isimu na fasihi ya Kiswahili. Ongezeko

hilo, lilitokea baada ya uongozi kuona umuhimu wa kuomba kibali cha kuongeza walimu kutoka wizara maalumu inayohusika na masuala ya elimu. Walimu ambao wanafundisha kozi mbalimbali zikiwemo kozi za Kiswahili. Hivyo, mwaka 2015 MNMA kilipata sura mpya kwa kuwa kilifanikiwa kuwahamisha watumishi kutoka katika idara na sekta mbalimbali za serikali nchini ambao walihamia chuoni hapo. Watumishi hao 6 kati yao walibobea katika kozi za isimu na fasihi ya Kiswahili. Tangu wakati huo, MNMA kimepiga hatua kubwa katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili.

Juhudi za kukiimarisha Kiswahili MNMA hazikuishia hapo, kwani uongozi wa chuo uliendelea kuomba walimu wa Kiswahili kila uchao. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaotaka kusoma kozi mbalimbali za Kiswahili ambao walidahiliwa kila mwaka. Hivyo, kupatikana kwa walimu hao, kulisaidia sana kuweka msukumo zaidi wa kukiimarisha Kiswahili. Kwa mnasaba huo, ni dhahiri kwamba MNMA kimeanza kukikubali Kiswahili na kukipa nafasi inayokaribiana na ile ya Kiingereza.

**Kuanzishwa kwa Idara ya Lugha na Fasihi**

Kuanzishwa kwa Idara ya Lugha na Fasihi ya Kiswahili katika MNMA kumeimarisha sana hali ya Kiswahili chuoni hapo na taifa la Tanzania kwa ujumla. Kiswahili kinafundishwa katika idara hii kikiwa kinajumuishwa pamoja na Kiingereza. Kabla ya kuanzishwa kwa idara hii, kozi za Kiswahili na Kiingereza zilijumuishwa ndani ya Idara ya Elimu. Idara ya Lugha na Fasihi ya Kiswahili imeunganisha kozi za isimu na zile za fasihi ya Kiswahili pamoja na kozi za isimu na fasihi ya Kiingereza. Bila shaka, hii ingekuwa bora zaidi iwapo idara hii ingetenganishwa na ile ya Kiingereza ili ziwe idara mbili tofauti. Kufanya hivyo, kungerahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

Licha ya upungufu huu, Idara ya Lugha na Fasihi ya Kiswahili inapigania nafasi ya Kiswahili na kuandaa mitaala ya kufundishia kozi zote za isimu na fasihi ya Kiswahili. Hivi sasa wahadhiri wanapewa fursa ya kufundisha kozi ambazo wamebobea hali ambayo inachangia katika kukuza viwango vya umilisi wa Kiswahili kutokana na utafiti katika vitengo vya isimu na fasihi ya Kiswahili. Vilevile, idara inasaidia katika maandalizi ya semina na warsha za Kiswahili pamoja na kuwahimiza walimu na wanafunzi kuendeleza masomo yao katika viwango vya uzamili na uzamivu wanaotaka kwenda masomoni kila mwaka. Si hayo tu, bali idara hii pia inafanya kazi kubwa ya kuwahamasisha walimu pamoja na wanafunzi kujiunga katika vyama mbalimbali vya kukikuza na kukiendeleza Kiswahili kwa mfano: CHAUKIDU, CHALUFAKITA, CHAKAMA na vingine vingi. Pia, Idara ya Lugha na Fasihi inajitahidi kuwahimiza walimu na wanafunzi, kuhudhuria makongamano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

**Kufanyika kwa Tafiti za Kitaaluma**

Kiswahili kimepata mafanikio makubwa katika nyanja za utafiti. Hivi katika maktaba ya MNMA kuna tasnifu kadhaa zilizoandikwa kwa Kiswahili. Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa hapo zamani ambapo tasnifu nyingi ziliandikwa kwa Kiingereza. Baadhi ya tasnifu za Kiswahili zilizoko maktabani ni na tasnifu ya: Adolph (2014) inayohusu Utohozi wa Nomino za Kiswahili na Athari zake katika Ngeli za Kihaya, Adolph (2019) inayohusiana na Utohozi wa Istilahi za Kiingereza katika Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Taaluma za Tiba na Kompyuta, Juma (2021) iliyoshughulikia Ulinganishi wa Kiisimu baina ya Kipemba na Kingazija, Haonga (2022) iliyochunguza Ulinganishi wa Kiisimu kati ya Kiswahili Sanifu na Kiswahili cha Kongo, Nyangaywa (2023) ambayo ilijikita katika Uchunguzi wa Matumizi ya Istilahi za Kiswahili za Programu za Simu za Mikononi kwa Wazungumzaji wa Kiswahili Nchini Tanzania, Isindikiro (2023) inayohusu Tathmini ya Mchakato wa Uundaji wa Istilahi za Kiswahili na Ukubalifu wa Istilahi Hizo kwa Watumiaji pamoja na tafiti mbalimbali. Aidha, zipo tafiti kadhaa zinazoendelea kufanyika kwa minajili ya kuchapisha makala

mbalimbali za kitaaluma. Hii ni katika jitihada za kukiimarisha Kiswahili ndani ya MNMA ambapo walimu na wanafunzi wanapata fursa ya kwenda maktaba na kujisomea.

Ni bayana kuwa wataalamu hawa wanaofanya tafiti mbalimbali, wanachangia katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili. Wataalam hawa wameandika makala nyingi katika majarida mbalimbali kama vile: Mulika, Kioo cha Lugha na Kiswahili ya TATAKI Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Jarida la Mwanga wa Lugha la Chuo Kikuu cha Moi nchini Kenya, CHALUFAKITA, CHAKITA, Journal of Kiswahili and Other African Languages na mengineyo. Makala mbalimbali zinazochapishwa kutokana na utafiti kuhusiana na lugha na fasihi ya Kiswahili ni muhimu kwa vizazi vya baadaye kwa vile ni msingi imara wa kuikuza na kuiendeleza taaluma ya Kiswahili. Aidha, kupitia machapisho hayo, wanafunzi wanaosoma kozi mbalimbali za Kiswahili, wameonekana kuingia kwa wingi maktabani kwa ajili ya kujisomea. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwepo kwa machapisho hayo ambayo yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili kama asemavyo mtoa taarifa mmoja:

> Kazi mbalimbali zilizopo maktabani ambazo zimeandikwa kwa Kiswahili, zimewasaidia sana wanafunzi wanaosoma kozi mbalimbali za Kiswahili. Kabla ya machapisho hayo baadhi ya wanafunzi waliiona maktaba kama kituo cha polisi.

Maelezo hayo, yanadhihirisha umuhimu wa machapisho hayo ya Kiswahili katika maktaba ya MNMA. Kuwepo kwa machapisho mengi kuhusu Kiswahili kwa Kiswahili kwa kweli kumewahamasisha wanafunzi kusoma somo la Kiswahili. Hapo awali wanafunzi waliambaa maktaba kwa vile machapisho mengi yalikuwa katika Kiingereza.

**Udhamini wa Masomo**

Moja kati ya hatua kubwa na muhimu iliyofanywa na MNMA katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili ni kutoa udhamini wa masomo. Katika kila idara kuna utaratibu ulio bayana kwa wafanyakazi wote wanaotaka kwenda masomoni kila mwaka. Utaratibu huo umeelekezwa kwa wakuu wa idara zote. Hivi sasa kuna utaratibu ambao umewekwa chuoni kuhakikisha kuwa kila idara inatoa fursa kwa wafanyakazi wanaotaka kujiendeleza kimasomo. Kwa hivyo, kila mwaka chuo hutenga kiasi cha pesa kuhakikisha kuwa idadi maalumu ya wafanyakazi wanakuza ujuzi wao wa kufanya kazi kwa weredi. Kwa njia hii, idara ya Kiswahili inaendelea kupata wataalamu ambao wanaweza kuchapuza maendeleo ya Kiswahili chuoni na nchini kwa ujumla.

Baada ya watumishi wa MNMA kujiorodhesha kwenye idara zao, vikao vingine vya majadiliano na uongozi wa chuo vinafuata. Sababu ya kufanya hivyo ni kwamba: mosi, chuo hakina uwezo wa kuwadhamini watumishi wote waliojiorodhesha na kuingia kwenye mpango. Pili, chuo hakiwezi kuwapeleka watumishi wote walioomba kwenda masomoni kwa wakati mmoja kwa kuwa, taratibu nyingine lazima ziendelee. Bila shaka kutakuwa na uhaba wa watumishi katika sekta mbalimbali.

Hivyo, kuna utaratibu ambao unafuatwa ili kuwateua watumishi wachache tu ambao huwekwa kwenye mpango huo kwa awamu. Utaratibu huu uko wazi ambapo kila mtumishi anauelewa na anapaswa kuufuata. Uteuzi huo wa watumishi kwenda masomoni unafanywa kwa ushirikiano wa wakuu wa idara pamoja na uongozi wa chuo kupitia vikao vyao mbalimbali. Kipaumbele cha kwanza cha uteuzi wa watumishi hao ni uzoefu wao kazini. Vilevile, endapo mtumishi atapata udhamini wake binafsi nje ya udhamini wa chuo huruhusiwa kwenda masomoni na pia mara nyingine hutegemea uhitaji na uhaba mkubwa kulingana na kozi husika. Kwa kuwa kuna vigezo vilivyo bayana kwa kila mtumishi, vimesaidia sana kurahisisha na kuondoa upendeleo, sintofahamu na manung’uniko kwa baadhi ya watumishi.

Idara ya Lugha na Fasihi ni mojawapo ya idara zilizopata mafanikio makubwa kupitia mpango huo. Tunafikia suluhisho hilo kwa kuwa Kiswahili kimezidi kuimarika, kukua na kuendelezwa zaidi. Kama ambavyo tumetangulia kusema hapo kabla kwamba, MNMA kilianza kuhuika, kuimarika na kukua zaidi kuanzia mwaka 2015. Kabla ya hapo hakukuwa na mhadhiri hata mmoja wa Kiswahili ambaye alikuwa na shahada ya Uzamivu. Mpango huo umechangia pakubwa kukuza na kuendeleza Kiswahili MNMA. Kwa ujumla hivi sasa tunao wahadhiri saba (7), mhadhiri mwandamizi mmoja (1) ambapo kwa pamoja wamebobea katika isimu na fasihi ya Kiswahili. Nafasi kwa wahadhiri kujiendeleza kimasomo ni muhimu katika kuimarisha ufundishaji wa taaluma ya Kiswahili kwa vile wanafunzi wengi wanaweza kujisajili kusomea kozi za taaluma ya Kiswahili.

**Ongezeko la Wanafunzi**

Kuna utitiri wa wanafunzi wanaodahiliwa kila mwaka wanaoomba kusoma kozi za ualimu zikiwemo za isimu na fasihi ya Kiswahili. Ongezeko hilo limetokea baada ya MNMA kuchukua juhudi za makusudi za kukiimarisha na kukikuza Kiswahili. Kabla ya mwaka 2015 MNMA kilikuwa na majengo machache tu katika bewa la Kivukoni. Hivyo, uchache wa majengo ulikifanya chuo kishindwe kudahili wanafunzi wengi ambao walikuwa na uhitaji kwa kipindi hicho. Ongezeko la wanafunzi wa Kiswahili chuoni unatokana na kuwepo kwa majengo na miundombinu imara, wahadhiri wa kutosha, kuimarishwa kwa mitaala pamoja na hadhi ambayo somo la Kiswahili linapewa na chuoni hicho. Mathalani, kutangazwa kwa Kiswahili na Shirika la UNESCO kuwa mojawapo ya lugha za kimataifa na kutengewa siku maalum ya maadhimisho yake; 7/7 ya kila mwaka.

Hali hiyo imepokelewa kwa mikono miwili na uongozi wa MNMA ambapo imeshajiisha kufanya juhudi za kuongeza majengo ili kukidhi idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na chuo hicho. Kiujumla uimarishaji wa kozi, miundombinu yakiwemo majengo, wahadhiri na hata machapisho ya Kiswahili ndio umechangia ongezeko la wanafunzi chuoni. Umaarufu wa Kiswahili bila shaka umechangia katika umaarufu wa chuo nchini Tanzania na ulimwenguni kote.

Baadaye kutokana na juhudi za serikali pamoja na uongozi wa MNMA uliona umuhimu wa kuongeza majengo. Jambo hilo lilisukumwa kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi. Kwani ilibainika kwamba, baadhi ya wanafunzi wenye sifa wanakosa nafasi kutokana na ukosefu wa majengo. Hivyo, chuo kilianza kukua kwa kuongezwa majengo mapya na kukarabati yale ya zamani yaliyokuwa yamechoka. Majengo hayo yamejumuishwa kwa pamoja yakiwemo yale ya mihadhara, ofisi za watumishi, mabweni ya wanafunzi pamoja na maktaba. Mpaka sasa tunapoandika makala hii katika kampasi ya Kivukoni kuna majengo ya kutosha ya mihadhara, bweni 1 jipya la wasichana, ofisi kadhaa za wafanyakazi na maktaba kubwa ya kisasa ambayo inaendelea kujengwa. Hivyo, utanuzi huo wa majengo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi.

Kwa upande wa kampasi ya Karume ilioko Bububu Unguja, mchakato wa ujenzi unaendelea. Tunategemea muda sio mrefu kukamilika kwa ujenzi wa bweni moja kubwa kwa ajili ya wanafunzi wa kike na wa kiume. Bweni hilo litakapomalizika litakuwa na uwezo wa kuchukua karibu wanafunzi elfu mbili (2000). Ni wazi kwamba jengo hilo litakapokamilika, litasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya makazi kwa wanafunzi wanaoishi mbali na maeneo ya chuo. Matokeo yake idadi ya wanafunzi wa Kiswahili watakaodahiliwa itaongezeka.

**Mchango wa Wahadhiri katika Makongamano na Vyombo vya Habari**

Wahadhiri/wahadhiri wasaidizi/wahadhiri waandamizi na wanafunzi wa MNMA wako mstari wa mbele katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili. Mchango wao huo, unajidhihirisha kupitia

makongamano na mijadala mbalimbali inayoandaliwa na mabaraza ya Kiswahili kama vile BAKITA na BAKIZA pamoja na vyama mbalimbali vya kukuza na kuendeleza Kiswahili kitaifa na kimataifa. Mathalani, CHAUKIDU, CHALUFAKITA, CHAKITA, na CHAKAMA. Kupitia mabaraza na vyama hivyo, wahadhiri na wanafunzi wa MNMA wanapata fursa ya kuhudhuria katika makongamano na mijadala inayohusu lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, wahadhiri na wanafunzi hao wanakutana na maprofesa, madaktari, wanahabari, watafiti, nguli, washititi pamoja na wadau wote wanaokienzi Kiswahili.

Wadau wote hao, wanaohudhuria makongamano hayo mbali na Tanzania, wanatoka katika nchi nyingine mbalimbali zikiwemo: Marekani, Ujerumani, Japani, Uswidi, Kenya, Uganda, Komoro, Italia, China na nyingine nyingi. Aidha, katika makongamano hayo mbali na mambo mengine, mijadala na makala mbalimbali huwasilishwa. Kwa mantiki hiyo, wahadhiri na wanafunzi wa MNMA nao wanapata nafasi ya kushiriki na kutoa maoni yao mbalimbali kuhusu mada zinazowasilishwa. Hivyo, ni dhahiri kwamba wahadhiri na wanafunzi hao wanajijengea uwezo na kupata maarifa ya kutosha juu ya mada mbalimbali za Kiswahili zinazowasilishwa. Makongamano hayo hutoa fursa kwa wahadhiri na wanafunzi kunoa ujuzi wao katika stadi za Kiswahili na pia kupanua soko lao kiajira.

Vilevile, wahadhiri wa MNMA wanatoa mchango mkubwa katika kukiendeleza na kukikuza Kiswahili kwenye vyombo vya habari. Kwani, wanachangia makala mbalimbali za kitaaluma katika vyombo hivyo. Vilevile, wanajadili masuala mbalimbali ya matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha na kukemea matumizi mabovu yanayoichafua lugha adhimu ya Kiswahili. Sanjari na hilo, wahadhiri hao wanafafanua juu ya istilahi faafu zinazotumiwa katika Kiswahili. Wataalam wa Kiswahili chuoni MNMA wamepata umaarufu nchini na sasa wanaalikwa na vyombo vya habari kuchangia katika mijadala kuhusiana na lugha na fasihi ya Kiswahili. Mathalan wanahusishwa katika uundaji na usanifishwaji wa istilahi za Kiswahili kuambatana na ukweli kuwa Kiswahili kama lugha yoyote hai inafaa kukua kimsamiati kadiri jamii inavyokua kijamii, kisayansi na kiteknolojia. Wahadhiri hao hualikwa katika kipindi cha lulu za Kiswahili - TBC ajili ya kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi na sanifu ya Kiswahili. Kipindi hicho hurushwa hewani na TBC kila Jumamosi saa 2 asubuhi.

**Changamoto za Ukuzaji wa Kiswahili**

Licha ya hatua mbalimbali za makusudi zilizochukuliwa na MNMA katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili, kwa mujibu wa wasailiwa, bado kuna changamoto katika harakati za kukiendeleza Kiswahili katika MNMA kama ifuatavyo.

**Uchache wa Vitabu, Majarida na Majengo**

Licha ya jitihada za kuongeza idadi ya machapisho, kungali na uhaba wa machapisho hasa katika kozi mahsusi. Hakuna vitabu vya maeneo mengine ya isimu kama vile isimujamii na isimu-historia. Zaidi ya vitabu hivyo pamoja na tasnifu chache zilizoandikwa kwa Kiswahili hakuna vitabu vingine katika uwanja huo, ambavyo vinakidhi haja ya matumizi kwa wanafunzi wote wanaosoma Kiswahili katika MNMA. Vitabu vya Kiingereza viko vingi lakini kama tulivyotangulia kusema kwamba, baadhi ya wanafunzi hawana umilisi wa kutosha wa lugha ya Kiingereza. Hivyo, wanashindwa kutafsiri na kutafuta visawe faafu katika Kiswahili. Kutokana na hali hiyo tunapendekeza kwamba, kozi za tafsiri ziingizwe katika mtaala wa masomo kuanzia shahada ya kwanza na kuendelea ili kuwahami wanafunzi na maarifa ya kutafsiri machapisho katika Kiingereza hadi kwa Kiswahili na

kwa njia hiyo kukuza machapisho muhimu katika Kiswahili. Aidha, hivi sasa kampasi hiyo inakabiliwa na tatizo la makazi ya wanafunzi wanaoishi mbali na chuo. Baadhi ya wanafunzi wanalazimika kupanga nyumba za watu binafsi ambazo ni ghali sana. Hali hii inawakatisha tamaa wanafunzi kwa kiasi fulani: kwa mfano mwaka 2021/2022 wanafunzi wa Kiswahili waliodahiliwa ni 72, mwaka 2022/2023 ni 62 na mwaka 2023/2024 waliodahiliwa 65. Hapo tunabaini kwamba idadi ya wanafunzi wa Kiswahili wanaodahiliwa inapanda na kushuka kila mwaka. Bila shaka hali hiyo imesababishwa na changamoto hiyo ya makazi. Hivyo, ni wazi kwamba ujenzi wa mabweni ukikamilika, kama ilivyoongelewa katika § 3.1.7 utasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya makazi kwa wanafunzi hao wanaoishi mbali na maeneo ya chuo. Matokeo yake idadi ya wanafunzi wa Kiswahili watakaodahiliwa itaongezeka.

**Kasumba ya Kikoloni**
Ipo kasumba (japokuwa ni kwa kiasi kidogo) ya kukishusha hadhi Kiswahili na kukikweza Kiingereza. Hali hii imetokana na sera ya lugha ya Kikoloni. Ingawa wakoloni ndio waliokisanifisha Kiswahili, walifanya hivyo kwa lengo la kukidhi maslahi yao ya kiuchumi. Wakoloni walikidunisha Kiswahili na kukinasibisha na watumwa pamoja na maboi. Kiingereza kilikwezwa, kutukuzwa na kufanywa lugha ya wasomi wachache wenye hadhi ya juu (Mbaabu, 2007). Mathalani, tumeshuhudia kwenye vikao mbalimbali mara nyingi tunapewa uhuru wa kuzungumza lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, kwa bahati mbaya baadhi ya watumishi hupendelea kutumia Kiingereza badala ya Kiswahili. Wanafanya hivyo ili wasije wakaonekana kwamba usomi wao una walakini. Hii ni kasumba inayowatafuna baadhi ya Watanzania kwani wanadhani kwamba kuzungumza Kiingereza ndio usomi.

Ni muhimu kutambua kwamba lugha zote duniani ni sawa, hakuna lugha ambayo ni nzuri dhidi ya nyingine. Kwani kila lugha ina uwezo wa kujitegemea na kuwasilisha utamaduni wake bila msaada wa lugha nyingine. Mawazo haya yanadhihirishwa na Wanjala na mwenzake (2013, p. 143) wanaposema:

> Kumekuwa na imani potofu kuwa kuna baadhi ya lugha ambazo ni zenye hadhi zikilinganishwa na nyingine. Imani hizi hazina msingi wowote kwani hakuna lugha inayoweza kujidai ujimbi dhidi ya nyingine.

Maelezo ya wataalamu hao yanasadifu barabara mawazo ya baadhi ya wanaokibeza Kiswahili na kukitukuza Kiingereza. Jambo hili, limeiathiri sana jamii na ndiyo maana baadhi ya watu wanakimbilia kuwapeleka watoto wao shule binafsi ili wakasome Kiingereza. Baadhi ya shule binafsi mara nyingi zinasisitiza zaidi matumizi ya Kiingereza kuliko Kiswahili matokeo yake vijana hao, wanapomaliza shule wanakosa msingi imara katika lugha ya Kiswahili.

**Ufadhili kwa Wahadhiri wa Kiswahili**
Wahadhiri wa Kiswahili katika MNMA wana uhitaji mkubwa wa kufadhiliwa pale wanapoalikwa katika makongamano mbalimbali ya Kiswahili. Mathalani, kwenye makongamano ya BAKIZA, BAKITA, CHAUKIDU, CHALUFAKITA, CHAKITA, CHAKAMA, na kadhalika. Inapendekezwa, uongozi wa MNMA pamoja na bajeti ndogo wanayotengewa wahadhiri hawa, uongozi unaombwa kutenga bajeti ya kutosha kila mwaka kwa ajili ya kuwawezesha wahadhiri wa Kiswahili kuhudhuria makongamano hayo kwa ajili ya kuzinoa bongo zao lakini pia kukiletea chuo heshima. Aidha, wahadhiri wanaozembea kuhudhuria makongamano hayo, wanasisitizwa kuhudhuria kutokana na sababau kuwa makongamano hayo yana faida lukuki. Baadhi ya faida hizo ni: kuwasilisha makala zao na maandiko mbalimbali ambayo ndiyo ngazi ya kupanda madaraja kwa wahadiri hao, kupata uzoefu kutoka kwa nguli wa Kiswahili na nguli wa nyanja nyinginezo, kupata fursa mbalimbali,

kubadilishana mawazo na wenzao, kufanya utalii, kujenga mtandao, waandishi vichipukizi kujengewa uwezo wa uandishi, kukuza ari ya kuandika, fursa ya wadau kuwasilisha mahitaji yao, kuweka mikakati mbalimbali, kujua historia na mchango wa nguli wa Kiswahili na kadhalika (Adolph, 2023).

**Hitimisho**

Makala hii imeeleza kuhusu hali ya Kiswahili katika vyuo vikuu huku tukijikita katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA). Tumebainisha mafanikio ambayo kwa namna moja au nyingine yamechangia katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili chuoni hapo. Kwani hivi sasa tunashuhudia mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali za Chuo hiki. Hii ni kutokana na ukweli usiofichika kwamba, mafanikio yote hayo yaliyopatikana, yametokana na juhudi za makusudi zilizofanywa na serikali pamoja na uongozi wa MNMA uliopo katika kukikuza na kukipa hadhi Kiswahili. Miongoni mwa mafanikio hayo ni matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano, upanuzi wa kozi, ongezeko la wahadhiri, kuanzishwa kwa Idara ya Lugha na Fasihi, kufanyika kwa tafiti za kitaaluma, udhamini wa masomo, ongezeko la wanafunzi na mchango wa wahadhiri katika makongamano na vyombo vya habari.

Inapendekezwa kuwa MNMA kiwe na mikakati ya kuwashawishi watumishi wote kutambua kwamba Kiswahili ni lugha inayojitegemea katika viwango vyote. Hivyo, kinatakiwa kitambuliwe kama lugha iliyo na hadhi sawa na lugha nyinginezo mfano lugha ya Kiingereza. Vilevile, moja kati ya mafanikio tuliyoyabainisha ni kuanzishwa kwa Idara ya Lugha na Fasihi. Idara hii ingekuwa muafaka zaidi kama ingetenganishwa zikawa idara mbili. Idara ya Kiswahili na idara ya Kiingereza, kila moja ikajitegemea. Endapo hili litatimizwa, idara ya Kiswahili itarahisisha kutatua baadhi ya changamoto tulizozibainisha.

Aidha, tunapendekeza MNMA kifikirie namna bora zaidi ya kukihuisha Kiswahili ili kilete tija zaidi. Chuo hicho kinaweza kushirikiana na idara ya Kiswahili, kuona umuhimu wa kuanzisha kozi ya kufundisha Kiswahili kwa wageni. Hii ni fursa adhimu ambayo kama ikifanikiwa, itasaidia kukitangaza MNMA na kuleta maslahi bora zaidi. Tumejaaliwa kuwa na eneo kubwa lenye mandhari mazuri ya bahari. Mandhari ambayo baadhi ya wageni kutoka nje wanayahusudu. Hivyo, ni jukumu la Chuo kuboresha miundombinu kwa kujenga madarasa ya kisasa ambayo yatatumika kwa ajili ya shughuli hiyo. Vilevile, tunapendekeza MNMA kikishirikiana na idara husika kiweze kufikiria kuwa na utamaduni wa kuendesha makongamano mbalimbali ya Kiswahili. Aidha, wahadhiri wa Kiswahili wanapoomba ufadhili wa kuhudhuria makongamano, basi wawezeshwe hata kwa kiasi kidogo. Mambo hayo yakifanikiwa Kiswahili kitazidi kukua na kutindimaa zaidi. Tunaamini kwamba mambo tuliyoyapendeza katika makala hii, yanaweza kuwa sio rahisi kwa ghafla kuyatekeleza yote kwa wakati mmoja. Hata hivyo, MNMA kinaweza kuyaweka akilini na kuanza kufikiria baadhi ya mapendekezo katika utekelezaji wake hatua kwa hatua.

**Marejeleo**

Adolph, E. (2023). “Ukuzaji na uenezaji wa lugha ya Kiswahili katika karne ya 21 kupitia maazimio, matamko na ushauri wa viongozi wa serikali katika MASIKIDU”. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *1*(1), 31-46.

Adolph, E. (2023, Disemba 14 – 16). Fursa zitokanazo na makongamano ya vyama vya kiswahili ndani na nje ya Tanzania. Makala isiyochapishwa, iliyowasilishwa kwenye kongamano la nane la kimataifa la CHAUKIDU, lililofanyika MS Training Centre for Development Cooperation (MS TCDC) Arusha – Tanzania.

Gibe, A. G. (1983). Tanzania's language police with special reference to Kiswahili as an educational medium. *Kiswahili*, *50*(1), 46-50.

Kiango, J. G. (2023, Julai 4). Kiswahili na wadau: fursa, changamoto kwa maendeleo endelevu. Makala isiyochapishwa, iliyowasilishwa kwenye kongamano la maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani, lililofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mark, A., & Jacktone, O. (2014). Kiswahili kama chombo cha kutangaza na kuuza vyombo vya habari nchini Kenya. *CHAKITA*, 87-97.

Massamba, D. P. B. (1995). Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. *Kiswahili katika kanda ya mashariki*, 1-11.

Marshad, H. A. (1993). *Kiswahili au Kiingereza nchini Kenya*. Jomo Kenyatta Foundation.

Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili origins and bantu divergence-convergence theory*. TUKI.

Mazrui, A. M., & Shariff, I. N. (1994). *The Swahili: idiom and identity of an African people*. Africa Word Press.

Mazrui, A. M, & Alamin, M. (1998). *The power of Babel: language and governance in the African experience*. University of Chicago Press.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya usanifishaji wa Kiswahili*. TUKI.

Mjawiri, M. M. (2016). Hali ya Kiswahili Zanzibar na mustakbali wake. *JAHAZI*, *1*, 17-25.

Morani, J. (2007). Hali ya Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya. *CHAKAMA,* 2-11.

Mutembei, A. (2011). Kukitandawazisha Kiswahili kupitia simu za kiganjani: tafakari kuhusu isimujamii. *Swahili Forum*, *18*, 198-210.

Mutembei, A. (2016). Utandawazi wa lugha za kiafrika: nafasi ya kiswahili sanifu katika Afrika inayobadilika. *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*, Daud Publishing Company Limited, 453-476.

Odeo, I. I., & Wamalwa, E. W. (2017). *Lugha na fasihi katika karne ya ishirini na moja*. Moi University Press.

Sharifu, I. N. (1988). *Tungo zetu*: *msingi wa mashairi na tungo nyinginezo*. The Red Sea Press Inc.

Walliman, N. (2011). *Research methods*: *the basics*. Routledge.

Wanjala, F. S., & Kavoi J. M. (2013). *Stadi za mawasiliano na mbinu za kufundisha Kiswahili*: *kwa wanafunzi, wanafunzi na walimu*. Serengeti Educational Publisher.